



ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI

GREDI YA 5 – 2026

TATHMINI ENDELEU

SHUGHULI ZA KISWAHILI (INSHA)

Muda: Dakika 40

Jumla ya Alama: 20

Mada

SHEREHE NILIYOHUJURIA

1. MFANO WA INSHA

Jumamosi iliyopita nilihudhuria sherehe ya harusi ya binamu yangu katika kijiji chetu. Siku hiyo ilikuwa ya furaha kubwa kwa familia yetu na marafiki.

Asubuhi mapema tulihamka na kuanza maandalizi. Mama na shangazi walipika vyakula vitamu kama wali, pilau, chapati na nyama. Watu wengi walifika wakiwa wamevaa nguo nzuri na zenye rangi mbalimbali.

Baadaye muziki ulianza kupigwa na watu wakaanza kucheza na kuimba kwa furaha. Watoto pia walicheza michezo na wengine walipiga picha ili kukumbuka siku hiyo muhimu.

Wageni walikaribishwa kwa chakula na vinywaji. Kila mtu alifurahia chakula na mazungumzo mazuri. Bwana na bibi harusi walionekana wenye furaha sana.

Mwisho wa sherehe tulimpongeza binamu yangu na kumtakia maisha mema ya ndoa. Nilifurahia sana kuhudhuria sherehe hiyo kwa sababu nilikutana na marafiki na jamaa wengi.

Kwa kweli ilikuwa siku ya kukumbukwa katika maisha yangu.

2. VIPENGELE VYA TATHMINI (VIGezo)

Insha itapimwa kulingana na vipengele vifuatavyo:

- Uelewa wa Mada
- Mpangilio wa Mawazo
- Matumizi ya Msamiati
- Sarufi na Tahajia
- Ubunifu na Uwasilishaji

3. RUBRIKI YA TATHMINI (CBC)

Kiwango	Maelezo
Kuzidisha Matarajio (4)	Mwanafunzi anaelewa mada vizuri sana, mawazo yamepangwa kwa mpangilio mzuri, anatumia msamiati mpana na sarufi sahihi.
Kufikisha Matarajio (3)	Mwanafunzi anaelewa mada na anawasilisha mawazo vizuri ingawa kuna makosa machache ya sarufi au mpangilio.
Kukaribia Matarajio (2)	Mwanafunzi anaelewa mada kwa kiasi lakini mawazo hayajapangwa vizuri na kuna makosa kadhaa ya sarufi.
Chini ya Matarajio (1)	Mwanafunzi haelewi mada vizuri, mawazo hayana mpangilio na kuna makosa mengi ya lugha.

4. RUBRIKI YA ALAMA (KWA KILA KIGezo)

Kigezo	Alama
Uelewa wa Mada	4
Mpangilio wa Mawazo	4
Matumizi ya Msamiati	4
Sarufi na Tahajia	4
Ubunifu na Uwasilishaji	4
Jumla	20

5. MWONGOZO WA UTOAJI WA ALAMA

Alama	Kiwango cha Umahiri
17 - 20	Kuzidisha Matarajio
13 - 16	Kufikisha Matarajio
9 - 12	Kukaribia Matarajio
0 - 8	Chini ya Matarajio

6. MFANO WA JINSI MWALIMU ANAVYOTDA ALAMA

Kigezo	Alama
Uelewa wa Mada	3
Mpangilio wa Mawazo	4
Msamiati	3
Sarufi	3
Ubunifu	3
Jumla	16 / 20

Kiwango: Kufikisha Matarajio